Kujenga “Makazi” Kwa wanawake wenye saratani Tanzania

Changamoto

Tanzania ina viwango vya juu vya saratani ya mlango wa kizazi na matiti katika dunia, ila ni hospitali moja tu katika nchi hii yenye idadi ya watu milioni 49 inatoa huduma maalumu ya matibabu hayo.Ocean Road Cancer Institute (ORCI) ambayo inapatikana Dar es Salaam inahudumia takribani wanawake 10,000 kila mwaka wenye saratani ya kizazi na matiti, asilimia 60 kati yao wanaishi nje ya mji mkuu(Dar es Salaam).Hospitali ya pili ya saratani imepangwa kufunguliwa mwaka 2016 katika Hospitali ya Bugando (BMC) jijini Mwanza,mji wa pili kwa ukubwa katika taifa, ambao unapatikana katika mwambao wa Ziwa Victoria

Pamoja na upatikanaji wa hospitali hizi, wanawake wengi wanaokutwa na saratani hawatafuti huduma,au wanasitisha huduma mara tu wanapoanza. Wengi wao hufia nyumbani.
Sababu? Wanaishi mbali sana na Hospitali,na hawana sehemu salama na nafuu ya kuishi ili kuhudhuria katika matibabu yao ya saratani.

Wanawake ambao hawana fedha za kulipia makazi/malazi kwa muda mrefu, au wale ambao hawana familia au marafiki jijini Dar es Salaam au Mwanza ambao wanaweza kuishi nao kwa muda zaidi, wanakabiliwa na changamoto ya kuwa na kambi nje au karibu na viwanja vya hospitali ambavyo sio makazi sahihi. Matokeo yake, wanawake wengi huamua kubaki nyumbani na kufa, badala ya kuvumilia kupata matibabu ya saratani katika mji ambao uko mbali na familia na nyumbani kwao katika maeneo ambayo hayaridhishi au hawawezi kumudu.

Suluhisho pendekezwa: Usanifu wa Kimataifa na Ushindani wa ubunifu.

Pink Ribbon Red Ribbon, American Cancer Society, George W. Bush Institute, HKS, Inc, Southern Methodist University (SMU) na T-MARC Tanzania inakusudia kujenga makazi (***makazi yanayokufanya ujisikie kama nyumbani***)kwa wanawake hawa, kama zilivyo/zinazofanana na zile za American Cancer Society Hope zilizopo nchini Marekani. Baada ya utafiti wa kina, tumepata gharama za kubuni na kujenga maeneo ya jijini Dar es Salaam na Mwanza kwa njia za ujenzi wa jadi ili kuwa na udhibiti wa kifedha. Hii imepelekea kutafuta ubunifu na gharama nafuu mbadala.

Tunajua wabunifu wametatua changamoto zinazofanana na hizi katika nchi zinazoendelea kwa kutumia vifaa vya ndani na mbinu endelevu za kiikolojia.Tunataka kuleta ubunifu huo kwaajili ya mpango wa hosteli bora , ili wanawake wenye saratani nchini Tanzania waweza kupata huduma wanazohitaji kuishi.

Tunazindua shindano la kimataifa la usanifu na ubunifu ili kutafuta njia/namna mpya ya ujenzi wa makazi(“makazi yanayokufanya ujisikie kama nyumbani”) ya wagonjwa wa saratani kwa kutumia njia za kibunifu,ufikiri mzuri,vifaa endelevu na ubunifu wa kivumbuzi.

Ushindani pendekezwa utachochea uvumbuzi na ubunifu, ambao utasababisha miradi na uwezo wa kuongeza upatikanaji wa tiba muhimu ambayo itaokoa maisha ya wanawake wengi. Ni matumaini yetu shindano hili pia litasaidia kuzalisha maslahi ya kutosha katika mawazo ya kushinda ili kusaidia uwekezaji katika ujenzi wao, kama vile uigiliziaji wa miundo katika maeneo mengine.

Malengo ya shindano

1. Kuhakikiksha **wanawake wengi zaidi wanakamilisha matibabu yao ya saratani** kwa kuwaondolea vikwazo vya kufikika;
2. Kutumia ubunifu kubuni na **kujenga uelewa mkubwa** wa saratani ya wanawake.
3. Kutoa fursa ya **kuendeleza malengo ya uwajibikaji wa kisanifu kijamii**
4. Kuwapa vijana/kuwatia moyo wasanifu,wabunifu na wanafuzi wa uhandisi ,ikihusisha wale wa kutoka Afrika,**nafasi ya kujenga maisha halisi ya mradi kazi** ambayo yatabadilisha maisha.
5. Kuwatia moyo washirika mpya kufanya kazi na Pink Ribbon Red Ribbon.

Maelezo ya shindano

Tarehe ya uzinduzi wa mashindano ni Aprili 7, 2016.

- waandaaji wa mashindano ni **Pink Ribbon Red Ribbon and the American Cancer Society**, kwa kushirikiana na **SMU, HKS, Inc, T-MARC Tanzania** and **TheGeorge W. Bush Institute**.
  - **Uwasilishaji utafuata moja ya vitu viwili:**
  - Moja kwaajili ya **mtaalamu** wa makampuni ya usanifu,ubunifu na uhandisi
  - Moja kwaajili ya wanafuzi wa chuo kikuu/ **wanafunzi wa shahada ya uzamili na wahitimu wa hivi karibuni** katika fani/tasnia hizo
- **Washiriki watashindania zawadi kwa kuwasilisha ubunifu wao wa kiwango cha juu zaidi kwa hosteli moja au zote**, na wanapaswa kuzingatia vigezo vyote kwa ujumla na vitu vya kipekee kwa kila eneo.
- Timu ya wataalamu inayoundwa na wasanifu na wabunifu wanaotambulika kimataifa (ikihusisha angalau Mtaalamu mmoja wa Kitanzania) na wataalamu wa saratani, **watatoa maamuzi, na kuchagua washindi katika makundi mawili.**

Pink Ribbon Red Ribbon: Kichocheo duniani

Pink Ribbon Red Ribbon®,**ina uhusiano na Taasisi ya George W. Bush, inaongoza katika uratibu wa kuokoa maisha ya wanawake na wasichana kutokana na saratani katika nchi zenye uhitaji mkubwa**. Ilizinduliwa Septemba 2011, ushirikiano na waanzilishi wengine;ni Serikali ya Marekani kupitia Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani kwa ajili ya UKIMWI (PEPFAR), Susan G. Komen® na Mpango wa Pamoja wa Umoja wa Mataifa wa kupambana na VVU / UKIMWI (UNAIDS). **Wakijikita katika kutoa huduma za kuzuia na matibabu ya saratani ya mlango wa kizazi na matiti**, Pink Ribbon Red Ribbon pia inashirikiana na makampuni na wanachama waanzilishi - Becton, Dickinson na Kampuni; Bill & Melinda Gates Foundation; Bristol-Myers Squibb Foundation; Caris Foundation; GlaxoSmithKline; Merck; na Qiagen - na kushirikiana na washirika, kama vile American Cancer Society, National Breast Cancer Foundation, LiveStrong Foundation, na GE Healthcare. Pamoja ushiriki wa serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali na mashirika ya kimataifa, na uongozi wa ngazi ya chini, matokeo ya ushirikiano katika nchi husika, mipango endelevu inayotoa fursa kwa wanawake na wasichana kupata huduma wanazohitaji kwaajili ya ustawi.

Jinsi tunavyofanya kazi

Kwa kuhamasisha/kukusanya rasilimali kutoka serikalini, mashirika ya kimataifa,Taasisi na makampuni, Pink Ribbon Red Ribbon na washirika wake hufanya kazi katika utoaji kamili huduma kuanzia kuzuia hadi kutoa uangalizi wa kina kwa:

Kuelimisha	Chanjo	Uchunguzi	Matibabu	Kuongeza	Mafunzo na vifaa
jamii kuhusu saratani ya matiti na mlango wa kizazi,na kuwawezesha wanawake kujikinga,kufanyiwa uchunguzi,matibabu,matunzo na msaada.	Kwa wasichana dhidi ya virusi vinavyosababisha saratani ya mlango wa kizazi.	Wanawake kwaajili ya saratani ya matiti na mlango wa kizazi,ikihusisha uchunguzi kwa njia ya visual with acetic acid (VIA) and HPV DNA.	Kwa wanawake ambao hawajapata saratani kwa njia rahisi na gharama nafuu; cryotherapy, and the loop electrosurgical excision procedure (LEEP).	upatikanaji wa huduma za kuokoa maisha uchunguzi, bidhaa na tiba, na kutoa msaada.	Watoa huduma wa umma na binafsi kufanya uchunguzi na kutibu saratani ya mlango kizazi na matiti

Tulikofika



Matokeo

- 42,045 - Idadi ya wasichana waliopatiwa chanjo ya dozi zote tatu(3) za chanjo ya HPV nchini Zambia na Botswana tangu 2011;
- 127,622 –Idadi ya wanawake waliofanyiwa uchunguzi saratani ya mlango wa kizazi nchini Zambia tangu2012;
- 10,097 – Idadi ya wanawake waliofanyiwa uchunguzi saratani ya mlango wa kizazi nchini Botswana tanguJuly 2012;
- 15,951– Idadi ya wanawake waliofanyiwa uchunguzi saratani ya mlango wa kizazi nchini Tanzania tangu July 2013;
- 5,228- Idadi ya wanawake waliofanyiwa uchunguzi wa saratani ya matiti nchini Tanzania tangu July 2013;

Ili kujua zaidi jinsi unavyoweza ukashirikiana na Pink Ribbon Red Ribbon, tembelea www.pinkribbonredribbon.org